TANGAZO LA SERIKALI Na. 24 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

## MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 28 la 2023

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita ya Mwaka 2025, na itasomwa kpamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita ya Mwaka 2023 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 6

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 6(2) kwa kufuta maneno "Bila kujali" na badala yake kuweka maneno "Bila kuathiri".

Marekebisho ya aya ya 13

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 13 kama ifuatavyo:

"Gharama za kuhifadhi chombo kilichokamatwa

**13.**-(1) Halmashauri itatoza gharama ya kuhifadhi ya kiasi cha shilingi elfu hamsini kila siku kwa chombo kilichobeba mzigo ulioshikiliwa baada ya kukamatwa ukisafirishwa bila kulipiwa ada au ushuru.

(2) Endapo, baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu tarehe ya kukamatwa kwa chombo chini ya aya ndogo ya (1), gharama ya kuhifadhi haijalipwa, Halmashauri inaweza kukiuza chombo hicho kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya

mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa chombo hicho baada ya kutoa gharama za kuhifadhi, gharama za mahakama na gharama za mnada.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo za (1) na (2), Mkurugenzi atapaswa, kabla ya kuuza chombo kilichokamatwa, kutoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza chombo hicho.".

Marekebisho ya Sehemu ya Pili

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kichwa cha habari chenye maudhui ya Sehemu ya Pili.

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*